SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI - OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

MWL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

ZANZIBAR

MEI, 2019

YALIYOMO

A.Utangulizi.....1
B.Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 5
G01-Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora..... 7
Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma..... 7
Programu ya Huduma za Serikali Mtandao..... 10
Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora 11
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora.....12
Taasisi zinazopokea Ruzuku.....15
Chuo cha Utawala wa Umma.....16
Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma.....17
G06: Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 19
Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma..... 15
G07: Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi..... 21
Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi..... 21
G08: Kamisheni ya Utumishi wa Umma..... 22
Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma..... 22

G09: Tume ya Utumishi Serikali..... 23
Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini..... 23
C.Muelekeo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2029 25
Vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 26
Malengo Makuu ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 27
E01- Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora 29
Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma..... 29
Programu ya Huduma za Serikali Mtandao..... 31
Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora..... 32
Programu ya Uendedshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora..... 33
Taasisi Zinazopokea Ruzuku 36
Chuo cha Utawala wa Umma 36
Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma..... 38
E02: Kamisheni ya Utumishi wa Umma..... 39
Programu ya Usimamizi ya Utumishi wa Umma. 39
E03: Tume ya Utumishi Serikalini..... 40
Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini 40
E04: Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 41

Programu ya ukaguzi na Udhibiti wa Fedha
na Serikali za Umma 41
E05: Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu
wa Uchumi..... 42
Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa
na Uhujumu Uchumi..... 42
D.Shukrani..... 43
E.Hitimisho..... 45
Kiambatanisho nam.1: Muhtasari wa
Upatikanaji wa Fedha 2018/2019 (katika ,000).. 47
Kiambatanisho nam.2: Makadirio ya Matumizi
kwa Mwaka 2019/2020 (katika ,000) 56
Kiambatanisho nam. 3: Makusanyo ya Mapato
Julai/Machi 2018/2019 na Makadirio ya
Mwaka 2019/2020 64
Kiambatanisho nam 4: Upatikanaji wa Fedha
za Maendeleo kwa Kipindi cha
Julai/Machi 2018/2019..... 65
Kiambatanisho nam 5: Mafunzo ya Watumishi
wa Ofisi Muda Mrefu na Mfupi 66
Kiambatanisho nam 6a: Jumla ya
Watumishi Kiwizara..... 69
Kiambatanisho nam 6b: Mashirika ya Umma..... 72
Kiambatanisho nam 6c: Shughuli za Tume
ya Utumishi Serikalini kuanzia July, 2018
Hadi Kufikia Machi, 2019..... 73

Kiambatanisho nam 6d: Watumishi walioajiriwa Kuanzia Julai, 2018 Hadi Kufikia Machi, 2019... 76
Kiambatanisho nam 6e: Malalamiko ya Watumishi kuanzia Julai–Machi 2018/19 79

HOTUBA YA WAZIRI NCHI OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHE.HAROUN ALI SULEIMAN (MBM) KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati, ili liweze kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii kwa ajili ya kuwasilisha taarifa ya utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 na mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa rehema zake tuweze kutekeleza vyema mipango

na malengo tuliojipangia kwa manufaa ya wananchi wetu na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Aidha, tunamuomba azidi kumpa nguvu, afya njema na umri mrefu Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein katika kuiongoza Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika,** niruhusu pia nitumie fursa hii kumshukuru Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa uongozi wake imara na wa mfano ambao umesaidia sana Wizara hii katika utekelezaji wa majukumu yake.

4. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuishukuru Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalumu za SMZ ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini na Makamo wake Mheshimiwa Zulfa Mmaka Mwakilishi wa viti maalum wa Vijana Mkoa wa Kusini Pemba, kwa maelekezo na mashirikiano mazuri waliyotupa wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/2019 na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi wa hali ya juu kama itakavyoelezwa hapa chini.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza aliekuwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Khamis Juma Maalim Mwakilishi wa Jimbo la Pangawe kwa kuteuliwa kwenye nafasi ya Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mmanga Mjengo Mjawiri Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani kuteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Mheshimiwa Simai Mohamed Said Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu George Joseph Kazi kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria. Kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuongoza Wizara hizo ni dalili tosha ya uwezo walionao katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo kwa lengo la kuleta maendeleo kwa nchi yetu ya Zanzibar.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba nimalizie kwa pongezi zifuatazo: kwanza kwako wewe binafsi Mhe. Spika, Naibu wako, na Wenyeviti wa Baraza kwa kuendelea kuliongoza Baraza letu kwa umahiri, uvumilivu mkubwa na bila kuyumba katika kusimamia kanuni tulizojiwekea. Pili, Mawaziri wenzangu na Wawakilishi wote kwa kazi nzuri

wanayofanya na kwa ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Tatu, na mwisho familia yangu na wapiga kura wa Jimbo la Uchaguzi la Makunduchi ambao wameendelea kunionyesha upendo na ushirikiano mkubwa hata pale ninapokuwa nimebanwa na majukumu ya kitaifa nje ya Jimbo langu la uchaguzi nawaahidi kushirikiana nao na kuhakikisha CCM inashinda katika Uchaguzi wa 2020.

7. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi hii ilikuwa na mafungu tisa kutoka kwa iliyokuwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kutokana na mabadiliko ya Wizara yaliofanywa hivi karibuni ya kutenganisha majukumu ya Sekta ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na sekta ya Katiba na Sheria kwa kuunda Wizara mbili tofauti, Ofisi hii kwa sasa inasimamia mafungu **G01**-Ofisi Kuu; **G06** Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; **G07**- Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; **G08** - Kamisheni ya Utumishi wa Umma na **G09**- Tume ya Utumishi Serikalini yanayoendelea kutekelezwa katika Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

8. **Mheshimiwa Spika,** mafungu manne yaliobakia **G02** - Mahakama Kuu, **G03** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, **G04** - Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na **G05** - Tume ya Kurekebisha Sheria yanaendelea kutekelezwa kupitia Wizara ya Katiba na Sheria.

9. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2018/2019 na mwelekeo wa bajeti ya mwaka 2019/2020 kama ifuatavyo.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 27,587,100,000 ambapo Shilingi 15,126,000,000 ni mishahara, Shilingi 11,411,100,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 1,050,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2019, jumla ya shilingi 19,771,126,691 zimepatikana sawa na asilimia 72. Aidha, Ofisi ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 761,453,000.

11. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2019, jumla ya Shilingi 9,411,695,000 zimepatikana sawa na asilimia 34 ya bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,697,911,000 zimetumika kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na shilingi 3,578,944,000 kwa matumizi mengineyo. Ofisi imepokea Shilingi 1,134,840,000 kwa ajili ya Chuo cha Utumishi wa Umma na Tume ya Maadili ya Viongozi. Kwa upande wa kazi za maendeleo Shilingi 130,000,000 zimepatikana. Pia, Ofisi ilikusanya Shilingi 24,000,000 kutokana na Ada ya Ukaguzi wa Mashirika na Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo **(angalia viambatanisho nam. 1,3 &4)**

12. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais- Utumishi wa Umma na Utawala Bora inatokana na iliyokuwa Ofisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ofisi ilikuwa na Mafungu tisa ambapo mafungu manne **G02** - Mahakama kuu, **G03** - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, **G04** - Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na **G05** - Tume ya Kurekebisha Sheria yamehamishiwa Wizara ya Katiba na Sheria. Mafungu **G01**-Ofisi Kuu; **G06** Ofisi ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; **G07**- Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; **G08** - Kamisheni ya Utumishi wa Umma na **G09**- Tume ya Utumishi Serikalini yanaendelea kutekelezwa katika Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Maelezo yafuatayo yanahusu utekelezaji wa mafungu matano (5) ya Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

G01- Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

13. **Mheshimiwa Spika,** Fungu la **G01** linahusisha Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma; Programu ya Huduma za Serikali Mtandao; Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORUUUB. Programu hizi zinasimamiwa na Katibu Mkuu.

14. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2019, hatua za utekelezaji wa programu za Fungu **G01** ni kama ifuatavyo:-

Programu kuu: Usimamizi na Uendelezaji wa Utumishi wa Umma

15. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya usimamizi wa Watumishi wa Umma ina programu

ndogo mbili na inatekelezwa kupitia Idara ya mipango Rasilimali Watu na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

16. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Mipango ya Maendeleo ya Watumishi yenye jukumu la kusimamia maendeleo ya rasilimaliwatu katika utumishi wa umma, imeratibu na kusimamia vikao vya wakurugenzi Uendeshaji, Utumishi na Maofisa Wadhamini, imewajengea uwezo maofisa Utumishi 87 na maofisa Sheria 27 na kuandaa mafunzo ya kujiandaa kustaafu kwa watumishi wa Umma Unguja na Pemba. Programu imeimarisha mfumo wa uwekaji wa taarifa za watumishi wa Umma na hadi kufikia Machi 2019, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina jumla ya Watumishi 43,408 waliomo katika Wizara na Taasisi mbali mbali Unguja na Pemba **(angalia kiambatanisho nam. 6a & 6b)**. Hadi kufikia Machi 2019, jumla ya watumishi 598 wamestaafu kazi baada ya kukamilisha muda wa utumishi Aidha, mafunzo kwa Maofisa Viungo (Focal Person) yametolewa kwa Wizara zote Unguja na Pemba. Vile vile, imefanya mapitio ya Mpango wa Rasilimaliwatu wa mwaka 2018/2019 na kuidhinisha Mpango wa Rasilimali Watu 2019/2020.

17. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ilipangiwa jumla ya Shilingi 357,900,000 na hadi kufikia Machi 2019, jumla ya Shilingi 220,554,950 zimepatikana sawa na asilimia 62. Kati ya hizo Shilingi 130,031,950 ni matumizi ya mishahara na Shilingi 90,523,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

18. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi kupitia programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi yenye jukumu la kusimamia Miundo, Mifumo ya Kitaasisi na Maslahi ya Watumishi, imeandaa na kutoa muongozo na fomu ya Upimaji Utendaji Kazi na muongozo na fomu ya Upandishwaji Vyeo katika Utumishi wa Umma. Idara imeandaa Mkataba wa utoaji huduma kwa Umma na kufanya mapitio ya Miundo ya Utumishi katika Wizara na Idara za SMZ, kuwasilisha Ripoti ya marekebisho ya Mishahara na kutoa mafunzo kwa watumishi katika ngazi mbalimbali za kiutendaji kuhusiana na masuala mbali mbali ya kiutumishi.

19. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 431,600,000 na hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 278,867,210 zimepatikana sawa na asilimia 65. Kati ya hizo Shilingi 188,212,210

ni matumizi ya mishahara na Shilingi 90,655,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Programu ya Huduma za Serikali Mtandao.

20. Mheshimiwa Spika, Idara ya Serikali Mtandao kupitia programu ya huduma za Serikali Mtandao imetoa miongozo miwili ya usimamizi wa TEHAMA katika Utumishi wa Umma na kufanya tathmini na ukaguzi wa mifumo na vifaa vya TEHAMA kwenye taasisi 21. Idara imewajengea uwezo watendaji katika ngazi mbali mbali kuhusiana na matumizi ya mifumo ya kompyuta na usalama wa mifumo, imetoa miongozo na barua pepe za Serikali na kuwapatia leseni ya matumizi ya mifumo. Aidha, Watendaji wa Idara wamepatiwa mafunzo mbali mbali ya kitaalamu ikiwemo *"Ethical Hacking"* na usanifu wa mifumo *(System Development),* usimamizi wa Ofisi, vifaa na miundombinu *(sopho).* Kwa kushirikiana na Kampuni ya Microsoft Idara imewapatia mafunzo watendaji 35 wa TEHAMA wa Taasisi mbali mbali za Serikali.

21. Mheshimiwa Spika, Idara imeendelea kuratibu mradi wa utoaji huduma za afya kwa njia za kielektroniki *(e-Health)* na mfumo wa ukusanyaji kodi *(e-Tax)* inayosimamiwa na kampuni ya Kichina ya ZTE.

22. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 665,100,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 394,666,170 zimepatikana sawa na asilimia 59. Kati ya hizo Shilingi 172,191,170 ni matumizi ya mshahara na Shilingi 222,475,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora

23. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2019, programu ya usimamizi wa utawala bora inayotekelezwa na Idara ya Utawala Bora imefanya tathmini ya kubaini kiwango cha uelewa wa dhana ya utawala bora kwa upande wa Pemba na kufanya makongamano mawili ya kitaifa Unguja na Pemba yenye lengo la kuimarisha utawala bora. Aidha, Elimu kwa walimu 175 wanaosomesha somo la uraia imetolewa na kutayarishwa na kurusha hewani vipindi vya redio na televisheni pamoja na kutoa elimu kwa madiwani na watendaji katika mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya Unguja na Pemba. Idara imechapisha na kusambaza nakala 1,714 za Jarida la Utawala Bora katika Taasisi za Serikali, Taasisi binafsi na wananchi mnamo mwezi Januari, 2019.

24. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 309,220,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 199,429,350 zimepatikana sawa na asilimia 64. Kati ya hizo Shilingi 109,921,350 ni matumizi ya mshahara na Shilingi 89,508,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

25. Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inatekelezwa na programu ndogo tatu ambazo ni;- programu ya Uongozi na Utawala, programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti na programu ya Uratibu Shughuli za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Pemba.

26. Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya Wizara, fedha za programu kuu ya uendeshaji na uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019 zinasomeka katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

27. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2019, programu ya Uongozi na Utawala kupitia Idara ya Utumishi na Uendeshaji imeratibu vikao tisa (9) vya Kamati tendaji,vikao vitatu (3) vya Kamati ya Uongozi, vikao viwili vya Bodi ya Zabuni na kikao kimoja na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kuimarisha mashirikiano katika Sekta ya Utumishi wa Umma. Aidha, Mfumo wa Kuhifadhia Kumbukumbu Tuli za Ofisi wenye lengo la kuhifadhi kumbukumbu kwa muda mrefu umeimarishwa. Katika kuwajengea uwezo watumishi Mafunzo mbali mbali ya muda mrefu na mfupi yametolewa ndani na nje ya nchi na kuwapatia mafunzo ya awali watumishi wapya katika Chuo cha Utawala wa Umma (IPA). **(angalia kiambatanisho nam.5).** Aidha, huduma za utawala na uendeshaji zimetolewa.

28. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 1,733,800,000 hadi kufikia Machi 2019 Shilingi 1,217,793,965 zimepatikana sawa na asilimia 70. Kati ya hizo Shilingi 741,564,865 ni matumizi ya mishahara na Shilingi 476,229,100 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

29. **Mheshimiwa Spika,** kazi za uratibu wa mipango, sera na utafiti zinatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kupitia programu husika. Hadi kufikia Machi 2019, Mipango ya bajeti na ripoti za utekelezaji za robo mwaka zimeandaliwa, kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini na mfumo wa takwimu wa Ofisi. Aidha, semina kwa Wakurugenzi Utumishi, Mipango na Maofisa wadhamini pamoja na watendaji wa Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali imefanyika kwa kushirikiana na Taasisi za Kusaidia Asasi zisizo za Kiserikali (ZANSASP), kwa lengo la kujenga uelewa na kutoa mapendekezo ya kuifanyia mapitio Sera ya Utumishi wa Umma.

30. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 390,580,000 hadikufikiaMachi2019,Shilingi262,828,800 zimepatikana sawa na asilimia 67. Kati ya hizo, Shilingi 143,698,800 ni matumizi ya mishahara na Shilingi 119,130,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

31. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2019, programu ya uratibu wa shughuli za Ofisi, imeratibu shughuli zote za Ofisi kwa upande wa Pemba pamoja na ziara nne za viongozi wa Ofisi wakiwemo Waziri,

Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Katibu wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Vile vile imeratibu ziara tatu za Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum za SMZ. Aidha, imedhamini mafunzo ya Shahada katika fani ya uchumi na Stashahada katika fani ya rasilimaliwatu kwa watumishi wawili. Pia, imehudumia shughuli za uendeshaji wa ofisi na utawala.

32. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 1,041,800,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 586,033,900 zimepatikana sawa na asilimia 56. Kati ya hizo Shilingi 475,020,000 ni matumizi ya mishahara na Shilingi 159,557,400 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU.

33. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Taasisi 2 zinazopokea ruzuku ambazo ni:- Chuo Cha Utawala wa Umma na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hadi kufikia 31 Machi, 2019 Ofisi imepokea ruzuku ya Shilingi 1,134,841,441. Utekelezaji wa kazi katika taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

Chuo cha Utawala wa Umma

34. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2019, programu hii imetoa mafunzo elekezi kwa Watumishi wapya 1,560 kutoka katika Wizara na Taasisi za Umma Unguja na Pemba kuhusiana na Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayohusiana na Utumishi wa Umma. Aidha, kazi za utafiti katika Sekta ya Utumishi wa Umma zimefanyika ambapo maeneo saba ya Utafiti yameibuliwa yakiwemo Serikali Mtandao, Usimamizi wa Fedha, Teknolojia ya Habari, Usalama wa Taarifa na Kumbukumbu, Uhusiano wa Umma na ubadilishanaji wa taarifa, Mipango, Sera, Utafiti na Ununuzi.

35. **Mheshimiwa Spika,** miongozi mwa maeneo saba (7) ya utafiti yaliyoibuliwa maeneo mawili yameanza kufanyiwa utafiti ambayo ni Maadili ya Usimamizi wa Kumbukumbu na nafasi ya ushirikishwaji watumishi wa umma katika programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma. Mafunzo ya muda mrefu yametolewa kwa Watumishi wa Umma na Wananchi wengine ambapo jumla ya wanafunzi 1,510 wamepatiwa mafunzo katika Ngazi mbali mbali kati ya hao, Watumishi wa Umma 507 na Wananchi wengine 1,003. Jumla ya Watumishi wanane

wamepatiwa mafunzo katika ngazi na fani mbalimbali. Aidha, huduma za utawala na uendeshaji zimetolewa kama zilivyopangwa.

36. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 643,600,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 508,495,551 zimepatikana sawa na asilimia 79. Kati ya hizo Shilingi 483,945,551 kwa ajili ya matumizi ya mishahara na Shilingi 24,550,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Chuo kimekadiria kukusanya Shilingi 1,269,870,000 kutokana na malipo ya ada za wanafunzi. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 1,145,564,320 zimekusanywa sawa na asilimia 90.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

37. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2019, Tume ya Maadili ya Vingozi wa Umma imehakiki taarifa mbali mbali za mali na madeni ya viongozi wa umma na kupokea fomu za viongozi wapya walioteuliwa na wanaomaliza muda wao wa utumishi Serikalini. Katika kipindi hicho, jumla ya tuhuma 11 za uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi zimepokelewa na kufanyiwa kazi. Orodha ya viongozi waliowasilisha fomu hizo imechapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali (Tangazo Nam. 6 la Februari 2019).

38. **Mheshimiwa Spika,** Tume imetoa elimu kwa viongozi wa umma kuhusiana na umuhimu wa kuimarisha maadili na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kufanya mikutano ya kuitambulisha Tume kwa baadhi ya Mabaraza ya Vijana. Vipindi 10 vinavyozungumzia majukumu, uwezo wa Tume pamoja na wajibu wa Viongozi wa Umma vimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar. Tume imeadhimisha sherehe ya Siku ya Maadili tarehe 10/10/2018.

39. **Mheshimiwa Spika,** katika maadhimisho ya siku ya Maadili, shughuli mbali mbali za kukuza uelewa pamoja na kuhamasisha Viongozi na wananchi kutambua umuhimu wa Maadili katika kuimarisha utawala bora zilifanyika kupitia utenzi, ngoma za kiutamaduni na mchezo wa kuigiza. Ujumbe/Kauli mbiu ya Maadhimisho hayo ni *"tuimarishe uadilifu, uwajibikaji, haki za binaadamu na mapambano dhidi ya Rushwa kwa maendeleo ya Taifa"*

40. **Mheshimiwa Spika,** Tume imeimarisha miundombinu ya ofisi kwa ajili ya uwekaji wa Mfumo wa Kieletroniki utakaotumika kusajili taarifa za mali na madeni ya

viongozi na kuwapatia mafunzo ya muda mfupi Watendaji wake katika fani mbali mbali ikiwemo Kompyuta, matumizi ya Mfumo wa Ki-elektroniki na mafunzo ya *'Network Security'*. Lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha usalama wa mfumo wa usajili wa taarifa za mali na madeni mara tu utakapokamilika na kuanza kutumika.

41. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 737,400,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 626,345,890 zimepatikana sawa na asilimia 85. Kati ya hizo Shilingi 206,345,890 ni matumizi ya mishahara na Shilingi 420,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

G06: OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma

42. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ya fedha na Rasilimali za Umma kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi imefanya ukaguzi wa hesabu za mwaka 2017/2018 katika Wizara zote za Serikali, Taasisi mbali mbali za Serikali na Miradi ya maendeleo

inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu na muongozo wa ukaguzi. Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2016/2017 imekamilika na hatua zinachukuliwa za kuwasilisha taarifa hizo kwa Mamlaka husika kama kifungu cha 112 (5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 ilivyoagiza, ili hatimae, taarifa hizo ziweze kuwasilishwa katika kikao cha Baraza la Wawakilishi. Aidha, jumla ya watumishi 25 wamepatiwa mafunzo mbali mbali ya Ukaguzi. Kwa upande wa mafunzo ya muda mrefu jumla ya wafanyakazi 15 wanaendelea na masomo katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi.

43. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 3,022,200,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 2,685,275,134 zimepatikana sawa na asilimia 72. Kati ya hizo Shilingi 1,602,261,300 kwa ajili ya mishahara na Shilingi 1,083,013,834 kwa matumizi mengineyo.

G07:MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI

Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi.

44. Mheshimiwa Spika, progaramu hii ina lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya kuchukuwa hatua za kinga dhidi ya Rushwa na kufanya uchunguzi wa vitendo vya Rushwa. Hadi kufikia Machi 2019, jumla ya tuhuma 157 za makosa mbali mbali ikiwemo kuomba na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya Ofisi, matumizi ya mali za umma, kukwepa kulipa kodi, Rushwa katika zabuni zimeripotiwa. Kati ya tuhuma hizo majalada 31 yamefikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua za kisheria na kupelekwa Mahakamani. Aidha, hatua za utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi zimeanza kwa kutoa elimu kwa Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Umma

45. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, hatua zilizofikiwa ni kuwa tayari Mamlaka imeshatiliana saini na Wakala wa Majengo Zanzibar Mkataba kwa

ajili ya utayarishaji wa Michoro na nyaraka za Zabuni za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa jengo hilo na usimamizi. Kazi za usanifu na utayarishaji wa michoro ya jengo hilo tayari zimekwishaanza na kutarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei 2019, ambapo Ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kuanza mapema mwezi Julai 2019.

46. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 1,590,800,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 1,194,205,340 zimepatikana sawa na asilimia 75. Kati ya hizo Shilingi 681,877,499 ni matumizi ya mishahara na Shilingi 512,327,841 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 110,000,000 zimepatikana kwa ajili ya kazi za usanifu na usimamizi wa Ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

G08: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma

47. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi 2019, Kamisheni imejenga uelewa kwa Maafisa utumishi kutoka katika Wizara na Taasisi mbali mbali juu ya utumiaji wa Muongozo wa Usalama na Afya kazini katika

Utumishi wa Umma. Vile vile, Kamisheni imeshughulikia Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi Sita (6) kutoka katika Taasisi mbali mbali za Umma na sasa inaendelea kufanya Utafiti unaohusu Usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma. Pia, Kamisheni imefanya ukaguzi wa kawaida na Maalum katika Mashirika ya Umma 11, Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Tume nne (4) za Utumishi ili kuangalia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi katika kutekeleza masuala ya Kiutumishi. Aidha, Kamisheni imepokea Rufaa tatu (3) na Malalamiko matano (5) na kuzitolea uamuzi.

48. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 1,033,000,000 na hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 784,376,347.00 zimepatikana sawa na asilimia 76. Kati ya fedha hizo, Shilingi 482,706,902 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi 301,669,445 kwa malipo ya mishahara ya watumishi.

G09: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI
Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini

49. Mheshimiwa Spika, jumla ya nafasi za ajira 1,637 zimetangazwa katika Wizara na

Taasisi mbali mbali kupitia ZBC Redio na Televisheni, kufanyiwa usaili na kutolewa vibali vya ajira. Jumla ya wafanyakazi 1,637 wameajiriwa katika Taasisi mbali mbali za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. **(angalia kiambatanisho nam. 6c).** Tume imewaongezea muda wa utumishi Serikalini watumishi 14, kubadilisha kada watumishi 49 na kuwapandisha daraja watumishi 11. Aidha, ajira 20 za mkataba zimeidhinishwa na Watumishi saba (7) wamepatiwa likizo bila ya malipo. Vile vile, Tume imetoa vibali vya kustaafu kazi kwa hiari kwa watumishi 25, kustaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima watumishi 563 na kustaafu kazi kwa maradhi watumishi 32. Watumishi 372 wamethibitishwa kazi na Watumishi watano (5) wameacha kazi. **(angalia kiambatanisho nam.6d).**

50. Mheshimiwa Spika, jumla ya makosa ya kinidhamu ya Watumishi 15 yamewasilishwa na kujadiliwa na kutolewa maamuzi ambapo Watumishi 14 wamefukuzwa kazi baada ya kuthibitika kuwa wamefanya makosa ya kinidhamu na mtumishi mmoja amerejeshwa kazini. Malalamiko matatu (3) yamewasilishwa na kutolewa uamuzi, **(angalia kiambatanisho nam. 6e).**

51. Mheshimiwa Spika, programu hii imepangiwa jumla ya Shilingi 529,200,000. Hadi kufikia Machi 2019, Shilingi 404,283,255 zimepatikana sawa na asilimia 76. Kati ya hizo Shilingi 151,464,555 ni matumizi ya mishahara na Shilingi 252,818,700 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

C. MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

52. Mheshimiwa Spika, naomba sasa kutumia fursa hii kutoa maelezo ya muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

53. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais- Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutumia jumla ya Shilingi 12,405,500,000. Kati ya hizo, Shilingi 6,405,800,000 zimepangwa kutumika kwa ajili ya kulipia mishahara na stahiki mbalimbali za watumishi na shilingi 5,999,700,000 zimepangwa kutumika kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

54. Mheshimiwa Spika, Ofisi imepanga kutumia ruzuku ya Shilingi 1,703,100,000

kwa ajili ya taasisi mbili ambazo ni Chuo cha Utawala wa Umma na Tume ya Maadili ya Viongozi. Kwa upande wa kazi za maendeleo Shilingi 3,648,200,000 zimepangwa kutumika kutekeleza miradi ya maendeleo. Pia, Ofisi imepanga kukusanya jumla ya Shilingi 158,000,000 kuchangia mfuko mkuu wa Serikali **(angalia kiambatanisho nam 2 & 4).**

VIPAUMBELE VYA OFISI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

55. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

i. Kuanza ujenzi wa jengo la Mamlaka ya Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar;

ii. Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Taarifa za Uhakiki wa Mali na Madeni kwa Viongozi wa Umma;

iii. Kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mkakati wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma Zanzibar (ZPSRP); na

iv. Kuendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za Serikali Mtandao.

Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020

56. Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuweka miundo ya Taasisi na kusimamia mipango endelevu ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;

ii. Kuimarisha utendaji kazi katika utumishi wa umma;

iii. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kieletroniki katika shughuli na utoaji wa huduma;

iv. Kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali; na

v. Kuanzisha na kuimarisha *Government Portal.*

57. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha maelezo ya programu za Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ifuatavyo:-

58. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza Programu kuu nane kama ifuatavyo: i) Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma, ii) Programu ya Huduma za Serikali Mtandao, iii) Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora, iv) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORUUUB, v) Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma, vi) Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini vii) Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma na viii) Progamu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

59. Mheshimiwa Spika, Programu nne za mwanzo zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na Programu zilizobakia zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

E01- Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma

60. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya usimamizi wa Watumishi wa Umma ina programu ndogo mbili na zinazotekelezwa kupitia Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 programu hii imepanga kuratibu na kusimamia Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano 2017/2022 katika Utumishi wa Umma, kujenga uelewa wa Sera ya Mafunzo ya Utumishi wa Umma, kuratibu mafunzo ya Watumishi wa Umma na kuwapatia mafunzo Maafisa Utumishi. Aidha, kupitia programu hii, Idara itaendelea kuratibu mafunzo ya Wastaafu katika Utumishi wa Umma na kuhakiki taarifa za watumishi wa umma.

61. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 302,004,000. Kati ya

hizo, Shilingi 182,867,000 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 119,137,000 zitatumika kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2)**

62. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2019/2020, programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi imepanga kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Muongozo na Fomu ya Upimaji Utendaji Kazi na Upandishwaji Vyeo katika Utumishi wa Umma na kutoa mafunzo kwa Maafisa Utumishi na Maafisa Wadhamini kuhusu Sheria, Miongozo, Matoleo na Kanuni za Utumishi wa Umma. Vile vile, Idara itaendelea kuandaa na kutoa ripoti ya marekebisho ya Mishahara, kufanya mapitio ya Mishahara na Posho kwa Wizara na Taasisi za Serikali na kuadhimisha siku ya Utumishi wa Umma Zanzibar.

63. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 388,870,000. Kati ya hizo, Shilingi 252,932,000 kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 135,938,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2)**

Programu ya huduma za Serikali Mtandao

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, programu ya huduma za Serikali Mtandao, imepanga kuandaa miongozo mbali mbali ya usimamizi wa TEHAMA na utoaji wa huduma kwa wananchi na kuratibu na kusimamia uanzishwaji wa mifumo ya kielektroniki katika Ofisi mbali mbali. Aidha, kupitia programu hii, Idara itafanya tathmini na ukaguzi wa vifaa na mifumo ya TEHAMA katika taasisi za Umma, kuelimisha na kujenga uwezo kwa watendaji, wanasiasa na wananchi juu ya dhana na huduma za Serikali Mtandao na huduma zinazotolewa kwa njia za kielektroniki na kusimamia miradi ya Serikali Mtandao. Idara imepanga kuwajengea uwezo wa kitaalamu wa usanifu, usalama, na usimamizi wa mifumo watendaji wa TEHAMA ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia na kutoa ripoti ya hali halisi ya TEHAMA Zanzibar.

65. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 744,103,000. Kati ya hizo Shilingi 367,644,000 kwa mishahara

na stahiki za watumishi na Shilingi 376,459,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora

66. Mheshimiwa Spika, programu ya usimamizi ya Utawala Bora inasimamiwa na Idara ya Utawala Bora yenye jukumu la kusimamia masuala ya utawala bora. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Idara kupitia programu hii imepanga kuratibu na kusimamia utekelezaji wa utawala bora kwa taasisi zinazosimamia Utawala bora kwa kuongeza uelewa kwa jamii juu ya dhana ya utawala bora, kufanya makongamano, tathmini na kutayarisha jarida la utawala bora.

67. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 296,684,000. Kati ya hizo, Shilingi 171,438,000 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 125,246,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina programu ndogo tatu na zinazotekelezwa kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu – Pemba.

69. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa programu ya uendeshaji na utawala wa ofisi, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imepanga kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, Idara itaimarisha usalama wa majengo, mazingira na afya za watumishi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa lengo la kutoa huduma bora kwa umma. Idara itaanzisha utaratibu wa kupima utendaji kazi kwa watumishi *(Performance Appraisal),* kuratibu zoezi la upandishwaji vyeo watumishi, kufanya zoezi la tathmini ya uwezo wa watendaji wa Wizara *(Capacity Needs Assessment)* na kuratibu uandaaji wa viongozi wa Ofisi. Aidha, Idara itasimamia taratibu za matumizi ya miongozo mbali

mbali ya kiutumishi, mfumo wa usimamizi wa fedha, ununuzi na ukaguzi wa ndani wa Wizara.

70. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 1,362,873,000. Kati ya hizo Shilingi 803,842,000 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 559,031,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 programu ya uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kuratibu na kuandaa mipango na bajeti ya Ofisi, miradi ya Sekta ya utumishi wa umma na utawala bora pamoja na kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Aidha, Idara itafanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Ofisi, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa awamu ya pili ya Mkakati wa Mabadiliko katika Utumishi wa Umma, masuala Mtambuka na kufanya mapitio ya Sera na Sheria ya Utumishi wa Umma na kuratibu na kufanya tafiti za Ofisi.

72. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 239,801,000. Kati ya hizo Shilingi 111,500,000 kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 128,301,000 kwa matumizi mengineyo. Vile vile, Shilingi 2,848,200,000 zimekadiriwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

73. **Mheshimiwa Spika,** programu ya uratibu na utekelezaji wa shughuli za Ofisi Pemba inayosimamiwa na Ofisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli zote za utawala na utumishi, mipango na bajeti zinazotekelezwa katika Ofisi hii.

74. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 584,065,000. Kati ya hizo Shilingi 400,777,000 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 183,288,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

TAASISI ZINAZOPOKEA RUZUKU
Chuo cha Utawala wa Umma

75. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020,Chuo cha utawala wa umma kitaendelea kutoa mafunzo ya kujenga uwez kwa Watumishi wa umma na Watumishi wa sekta binafsi, kuandaa na kutoa mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wanaoingia katika ajira kwa mara ya kwanza na kufanya utafiti katika Sekta ya Utumishi wa Umma pamoja na kutoa ushauri elekezi. Aidha, Chuo kitaandaa na kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi wa umma na wananchi wengine.

76. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utawala wa Umma kilianzisha mafunzo ya Shahada ya Kwanza katika fani za Rasilimaliwatu, Utunzaji Kumbukumbu na Nyaraka na Mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia katika mwaka wa masomo 2017 zikiwa na wanafunzi 110. Katika kuhakikisha kuwa Chuo kinaendesha mafunzo ya Shahada ya kwanza kwa ufanisi mkubwa kiliagizwa na Serikali kupitia Mpango wa Dharura kuajiri wakufunzi saba (7) katika kada ya Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia na kada ya Utunzaji Kumbukumbu na Nyaraka wenye sifa za Shahada ya Uzamivu

(PHD). Matangazo ya uajiri wa nafasi hizo tayari yameshatolewa na taratibu za uajiri zinaendelea. Aidha, Chuo kimewapeleka masomoni nje ya nchi wakufunzi wake watatu kuendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamivu na wawili katika Shahada ya Uzamili. Ni matarajio yetu kuwa mafunzo ya Shahada ya Kwanza yataendelea kutolewa tena ifikapo mwaka 2020 kwa kuzingatia zaidi shahada zitakazoendeleza Utumishi wa Umma katika SMZ.

77. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Miundo Mbinu ya kujifunzia Chuo kimekamilisha taratibu za ununuzi wa vifaa ikiwemo basi moja, vitabu rejea, *"Barcode na "Door Scanner"* na vifaa vyengine.

78. Mheshimiwa Spika, ili kukiwezesha Chuo kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi 725,200,000. Kati ya hizo Shilingi 684,300,000 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 40,900,000 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Chuo kimepanga kukusanya Shilingi 1,756,360,000 kutokana na malipo ya ada za wanafunzi **(angalia kiambatanisho nam 2 & 3).**

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

79. Mheshimiwa Spika, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2019/2020 itaendelea kupokea, kuhifadhi na kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma, kupokea malalamiko na kufanya uchunguzi wa uvunjwaji wa Sheria ya Maadili, kuhakiki taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma na kuelimisha viongozi wa umma na wananchi Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili. Vile vile, kuadhimisha siku ya maadili Duniani, kuwapatia mafunzo mbalimbali watumishi na kushiriki katika mikutano ya kimataifa, kikanda na kitaifa juu ya suala zima la maadili. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Tume inatarajia kukusanya jumla ya fomu 2,500 kutoka kwa Viongozi wa Umma na kufanya marekebisho ya jadweli ya Kwanza ya Sheria Nam. 4 ya mwaka 2015.

80. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe ruzuku ya Shilingi 977,700,000. Kati ya hizo Shilingi 296,200,000 kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi

681,500,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

E02: KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma,

81. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamisheni itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais kuhusu masuala ya kiutumishi pamoja na kuzisimamia Tume za Utumishi, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Wakala wa Serikali. Itafanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za umma, ukaguzi maalum na ukaguzi wa kushitukiza kuhusu usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma. Aidha, Kamisheni itapokea na kushughulikia rufaa na malalamiko dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma. Vile vile, Kamisheni imepanga kushughulikia na kuidhinisha Mapendekezo ya Miundo ya Utumishi mitano na Miundo ya Taasisi mitano itakayowasilishwa na Taasisi za Umma pamoja na kufanya utafiti kuhusu

changamoto za kiutumishi zilizo katika Utumishi wa Umma.

82. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya Shilingi 1,050,500,000 zitatumika. Kati ya hizo Shilingi 629,300,000 kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 421,200,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

E03: TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini

83. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Tume itaandaa na kusimamia shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki, kuendelea kusimamia haki na nidhamu za watumishi wa Serikali kwa kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi na rufaa za wafanyakazi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka za Nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa Tume. Aidha, Tume itaendelea kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada, kutoa

nyongeza za muda wa utumishi, likizo bila ya malipo na kustaafisha kisheria watumishi wa Serikali. Huduma za kiutawala na za uendeshaji zitatolewa

84. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 589,000,000. Kati ya hizo Shilingi 208,700,000 kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 380,300,000 kwa matumizi mengineyo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

E04: OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma

85. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi itaendelea kufanya majukumu yake ya kikatiba ya kukagua hesabu za Serikali na Taasisi zake zote kwa kutumia viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa pamoja na kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi.

86. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 3,962,900,000. Kati ya hizo Shilingi 2,172,900,000 kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 1,790,000,000 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 158,000,000 zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali **(angalia kiambatanisho nam 2 & 3).**

E05:MAMLAKA YA KUZUWIA RUSHWA NA UHUJUMU WA UCHUMI

Progamu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

87. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kupitia programu hii Mamlaka itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi na kufanya uchunguzi wa makosa mbalimbali ya rushwa na uhujumu wa uchumi. Mamlaka itaratibu na kutekeleza Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi pamoja na kuelimisha jamii juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi.

88. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 2,861,400,000. Kati ya hizo Shilingi 1,095,000,000 kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 966,400,000 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 800,000,000 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo **(angalia kiambatanisho nam 2).**

D. SHUKRANI

89. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 katika utekelezaji wa majukumu yetu. Shukurani za pekee ziwaendee Washirika wa Maendeleo walioendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango yetu ya uimarishaji sekta ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Washirika hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Benki ya Dunia *(World Bank),* Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuzuia

Uhalifu na Madawa ya Kulevya (UNODC) na Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (AAPAM).

90. Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru viongozi wenzangu na nikianza na Nd. Yakout Hassan Yakout, Katibu Mkuu, Nd. Seif Shaaban Mwinyi Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Tume na Kamisheni na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi hii, Wakuu wa Vitengo pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake kwa kuendelea kujituma kwa juhudi na maarifa katika kutekeleza malengo na majukumu ya Ofisi yetu. Vile vile, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Idara Kuu ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wakala wa Serikali Mtandao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Taasisi ya Makatibu Muhutasi Tanzania (TAPSEA).

91. Mheshimiwa Spika, tunawashukuru wahusika wote wa sekta ya utumishi wa umma na utawala bora ambao wametupatia ushirikiano wa kutosha katika kuendeleza sekta hii. Shukurani zangu za pekee nazitoa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali

na wafanyakazi wote kwa kuchapa vizuri hotuba hii.

E. HITIMISHO

92. Mheshimiwa Spika, Naomba nimalizie kwa kukumbusha kuwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inayo dhima ya kuhakikisha masuala yanayohusu utoaji wa huduma kwa wananchi yanasimamiwa ipasavyo pamoja na uimarishaji wa Maslahi ya Watumishi wa Umma, usimamizi wa Utawala Bora na kupiga vita vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar. Utekelezaji wa Mkakati wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma unalenga kuongeza ufanisi katika kufikia malengo ya MKUZA III, Dira ya 2020 ya Maendeleo ya Zanzibar pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu Duniani.

93. Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni ya kuiwezesha Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutekeleza vyema majukumu yake na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 17,756,800,000 kwa ajili ya matumizi ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, Shilingi

14,108,600,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na Shilingi 3,648,200,000 ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuruhusu Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 158,000,000 kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

94. Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho nam.1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha 2018/2019 (katika ,000)

MUHTASARI WA UPATIKANAJI WA FEDHA 2018 / 2019									
Programu Kuu/ Programu Ndogo	**Makadirio kwa Mwaka 2018/2019**					**Fedha zilizopatikana**			
	Jumla ya matumizi ya kawaida	**Mishahara na Maposho**	**Matumizi mengineyo**	**Jumla ya Fedha Zilizopatikana**	**Asilimia**	**Mishahara**	**Asilimia**	**Matumizi mengineyo**	**Asilimia**

Programu ya Uendelezaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma									
Programu ya Miundo na Mifumo ya Taasisi	431,600	250,600	181,000	278,867	65	188,212	75	90,655	50
Programu ya Mipango na Maendeleo ya Watumishi	357,900	198,900	159,000	220,555	62	130,032	65	90,523	57
Jumla ya Programu	**789,500**	**449,500**	**340,000**	**499,422**	**63**	**318,244**	**71**	**181,178**	**53**

Programu ya Huduma za Serikali Mtandao									
Programu ya Huduma za Serikali Mtandao	665,100	298,000	367,100	394,666	59	172,191	58	222,475	61
Jumla ya Programu	**665,100**	**298,000**	**367,100**	**394,666**	**59**	**172,191**	**58**	**222,475**	**61**
Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora									
Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora	309,220	142,220	167,100	199,429	64	109,921	77	89,508	54

Jumla ya Programu	**309,220**	**142,220**	**167,100**	**199,429**	**64**	**109,921**	**77**	**89,508**	**54**
Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora									
Programu ya Uongozi na Utawala	1,733,800	1,003,800	730,000	1,217,794	70	741,565	74	476,229	65
Programu ya Mipango, Sera na Utafiti	390,580	219,580	171,000	262,829	67	143,699	65	119,130	70

Programu ya Uratibu wa shughuli za Ofisi Kuu Pemba	1,051,800	806,400	245,400	634,577	60	475,020	59	159,557	65
Jumla ya Programu	**3,176,180**	**2,029,780**	**1,146,400**	**2,115,200**	**67**	**1,360,284**	**67**	**754,916**	**66**
Ruzuku Chuo cha Utawala wa Umma	643,600	605,000	38,600	508,495	79	483,945	80	24,550	64
Ruzuku Tume ya Maadili ya Viongozi	737,400	212,400	525,000	626,345	85	206,345	97	420,000	80
Jumla ya Ruzuku	**1,381,000**	**817,400**	**563,600**	**1,134,840**	**82**	**690,290**	**84**	**444,550**	**79**

Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma									
Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma	1,033,000	380,200	652,800	784,376	76	301,669	79	482,706	74
Jumla ya Programu	**1,033,000**	**380,200**	**652,800**	**784,376**	**76**	**301,669**	**79**	**482,706**	**74**

Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini									
Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa watumishi Serikalini	529,200	189,100	340,100	404,282	76	151,464	80	252,818	74
Jumla ya Programu	**529,200**	**189,100**	**340,100**	**404,282**	**76**	**151,464**	**80**	**252,818**	**74**

Programu ya Ukaguzi na Udhibi wa Fedha na Rasilimali za Umma									
Programu ya Ukaguzi na Udhibi wa Fedha na Rasilimali za Umma	3,709,869	2,159,869	1,550,000	2,685,275	72	1,602,261	74	1,083,014	70
Jumla ya Programu	**3,709,869**	**2,159,869**	**1,550,000**	**2,685,275**	**72**	**1,602,261**	**74**	**1,083,014**	**70**

Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi									
Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	1,590,800	876,000	714,800	1,194,205	75	681,877	78	512,327	72
Jumla ya Programu	**1,590,800**	**876,000**	**714,800**	**1,194,205**	**75**	**681,877**	**78**	**512,327**	**72**
JUMLA KUU	**13,183,869**	**7,342,069**	**5,841,900**	**9,411,695**	**71**	**5,388,201**	**73**	**4,023,492**	**69**
JUMLA YA G01	**4,940,000**	**2,919,500**	**2,020,600**	**3,208,717**	**65**	**1,960,640**	**67**	**1,248,077**	**62**
JUMLA G06 / G09	**6,862,869**	**3,605,169**	**3,257,700**	**5,068,138**	**74**	**2,737,271**	**76**	**2,330,865**	**72**
JUMLA YA RUZUKU	**1,381,000**	**817,400**	**563,600**	**1,134,840**	**82**	**690,290**	**84**	**444,550**	**79**

Kiambatanisho nam.2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2019/2020 (katika ,000)

MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA MWAKA 2019/20							
PROGRAMU KUU/ PROGRAMU NDOGO	**KAZI ZA KAWAIDA**			**KAZI ZA MAENDELEO**			
	JUMLA	**MISHAHARA NA STAHIKI**	**MATUMIZI MENGINEYO**	**SMZ**	**WAHISANI**	**JUMLA**	**JUMLA KUU**
Programu ya Uendelezaji na Usimamizi wa Watumishi wa Umma							
Miundo na Mifumo ya Taasisi	388,870	252,932	135,938			-	388,870
Mipango na Mandeleo ya Watumishi	302,004	182,867	119,137			-	302,004
JUMLA YA PROGRAMU KUU	**690,874**	**435,799**	**255,075**		**-**	**-**	**690,874**

Programu ya Huduma za Serikali Mtandao							
Huduma za Serikali Mtandao	744,103	367,644	376,459	100,000		100,000	844,103
JUMLA YA PROGRAMU	**744,103**	**367,644**	**376,459**	**100,000**	-	**100,000**	**844,103**
Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora							

Usimamizi wa Utawala Bora	296,684	171,438	125,246			-	296,684
JUMLA YA PROGRAMU	**296,684**	**171,438**	**125,246**	**-**	**-**	**-**	**296,684**
PROGRAMU YA Uendeshaji na Uratibu wa ORUUUB							
Uendeshaji na Utawala	1,362,873	803,842	559,031			-	1,362,873
Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti	239,801	111,500	128,301	200,000	2,548,200	2,748,200	2,988,001

Uratibu na Utekelezaji wa Ofisi Kuu Pemba	584,065	400,777	183,288			-	584,065
JUMLA YA PROGRAMU	**2,186,739**	**1,316,119**	**870,620**	**200,000**	**2,548,200**	**2,748,200**	**4,934,939**
Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma							
Usimamizi wa Watumishi wa Umma	1,050,500	629,300	421,200				1,050,500

JUMLA YA PROGRAMU	**1,050,500**	**629,300**	**421,200**	-	-	-	**1,050,500**
Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini							
Usimamizi wa Watumishi Serikalini	589,000	208,700	380,300				589,000
JUMLA YA PROGRAMU	**589,000**	**208,700**	**380,300**	-	-	-	**589,000**

Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma							
Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma	3,962,900	2,172,900	1,790,000			-	3,962,900
JUMLA YA PROGRAMU	**3,962,900**	**2,172,900**	**1,790,000**	-	-	-	**3,962,900**
Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi							

Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi	2,884,700	1,103,900	1,780,800	800,000		800,000	3,684,700
JUMLA YA PROGRAMU	**2,884,700**	**1,103,900**	**1,780,800**	**800,000**	-	**800,000**	**3,684,700**
Ruzuku Chuo cha Utawala wa Umma	750,200	684,300	65,900			-	750,200
Ruzuku Tume ya Maadili ya Viongozi	952,900	272,700	680,200			-	952,900
JUMLA YA RUZUKU	**1,703,100**	**957,000**	**746,100**	**-**	**-**	**-**	**1,703,100**

Jumla E01	**3,918,400**	**2,291,000**	**1,627,400**			-	**3,918,400**
Jumla ya Ruzuku E01	**1,703,100**	**957,000**	**746,100**			-	**1,703,100**
Jumla E01 na Ruzuku E01	**5,621,500**	**3,248,000**	**2,373,500**			-	**5,621,500**
Jumla ya E02+E03+E04+E05	**8,487,100**	**4,114,800**	**4,372,300**			-	**8,487,100**
Jumla kuu	**14,108,600**	**7,362,800**	**6,745,800**	**1,100,000**	**2,548,200**	**3,648,200**	**17,756,800**

Kiambatanisho nam. 3: Makusanyo ya Mapato Julai/Machi 2018/2019 na Makadirio ya Mwaka 2019/2020

MAKUSANYO YA MAPATO JULAI/MACHI 2018/2019				
IDARA /TAASISI	**MAKADIRIO 2018/2019**	**MAKUSANYO HALISI**	**ASILIMIA**	**MAKADIRIO 2019/2020**
G06 OFISI YA CAG	50,954,000	24,000,000	47	158,000,000
JUMLA	**50,954,000**	**24,000,000**	**47**	**158,000,000**
CHUO CHA UTAWALA WA UMMA	1,269,870,000	1,145,564,320	90	1,756,360,000
JUMLA	**1,269,870,000**	**1,145,564,320**	**90**	1,756,360,000

Kiambatanisho nam 4: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kwa Kipindi cha Julai /Machi 2018/2019

UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MAENDELAO KWA KIPINDI CHA JULAI /MACHI 2018/2019							
	FEDHA ZILIZOTENGWA			**FEDHA ZILIZOPATIKANA**			
JINA LA MRADI	**Mchango wa Serikali**	**Mchango wa Wahisani**	**Jumla**	**Mchango wa Serikali**	**Wahisani**	**Jumla kuu**	**ASILiMIA**
Mradi wa Serikali Mtandao	50,000,000		50,000,000			20,000,000	40
Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na uhujumu wa Uchumi	500,000,000		500,000,000	110,000,000		110,000,000	22
JUMLA	**550,000,000**	**-**	**550,000,000**	**110,000,000**	**-**	**130,000,000**	**24**

Kiambatanisho nam 5: Mafunzo ya Watumishi wa Ofisi Muda Mrefu na Mfupi

	MAFUNZO YA MUDA MREFU				
NAM	**KAZI/CHEO**	**JINSIA**	**ELIMU/FANI YA SASA**	**ELIMU/FANI ANAYOPENDEKEZWA**	**CHUO**
1	AFISA UENDESHAJI	M'ME	DEGREE P.A	MASTER PA	ZANZIBAR UNIVERSITY
2	AFISA UTUMISHI MKUU	M'ME	DEGREE P.A	MASTER HRM	OPEN UNIVERSITY
3	AFISA UTUMISHI MKUU	M'ME	DEGREE P.A	MASTER HRM	OPEN UNIVERSITY - TANZNIA
4	MCHAMBUZI WA COMPYUTA	M'KE	ADVANCED DIPLOMA IN COMPUTER SCIENCE	MASTER OF SCIENCE IN COMPUTEING	UGANDA TECHNOLOGY AND MANAGEMEN T UNIVERSITY

5	MKAGUZI WA HESABU ZA NDANI	M'ME	DEGREE	MASTER ACC	UNIVERSITY OF DODOMA
6	AFISA UFATILIAJI NA TATHMINI	M'ME	POST GRADUATE DIPLOMA IN REGIONAL PLANNING	MASTERS DEGREE IN PROJECT PLANNING, MONITORING AND EVALUATION	INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING
7	MCHAMBUZI KAZI MSAIDIZI	M'ME	DIPLOMA	DEGREE INTERNATIONAL RELATION	ZANZIBAR UNIVERSITY
8	AFISA UTUMISHI MSAIDIZI	M'ME	DIPLOMA ACCOUNTING	DIPLOMA HRM	CHUO CHA UTAWALA WA UMMA
9	KARANI MASJALA	M'KE	CERT. RECORD	DIPLOMA RECORD	CHUO CHA UTAWALA WA UMMA
	MAFUNZO YA MUDA MFUPI				
NAM	**KAZI/CHEO**	**JINSIA**	**ELIMU/FANI YA SASA**	**ELIMU/FANI ANAYOPENDEKEZWA**	**CHUO**

1	MKURUGENZI	M'ME	MASTER IN PUBLIC ADMINISTRATION	STRATEGIC HUMAN RESOURCE MANAGEMENT FOR IMPROVING ORGANIZATION PERFORMANCE	MOROGORO
2	MWANASHERIA	M'KE	MASTER IN LAW	LAW	CHINA
3	MWANASHERIA	MME	MASTER IN LAW	LAW	CHINA
4	MWANASHERIA	M'KE	DEGREE IN I R	GOOD GOVERNANCE	INDIA
MAFUNZO ELEKEZI					
	IDADI		**W'KE**	**M'ME**	
	10		3	7	

Kiambatanisho nam 6a: Jumla ya Watumishi Kiwizara

Nam	WIZARA	UNGUJA			PEMBA			JUMLA KUU
		W' UME	W' KE	JUMLA	W' UME	W' KE	JUMLA	
1	Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	178	86	264	32	16	48	312
2	Wizara ya Fedha na Mipango	510	356	866	81	37	118	984
3	Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora	246	186	432	68	43	111	543

4	Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo	126	119	245	49	12	61	306
5	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	389	241	630	105	46	151	781
6	Wizara ya Katiba na Sheria	357	173	530	119	53	172	702
7	Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Aamali	3326	3546	6872	1210	811	2021	8893
8	Wizara ya Afya	1338	1573	2911	782	477	1259	4170
9	Wizara ya Miundo mbinu, Mawasiliano na Usafiri	593	137	730	273	41	314	1044
10	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto	175	167	342	65	50	115	457

11	Wizara Habari, Utalii na Mambo ya Kale	444	422	866	76	47	123	989
12	Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati	623	149	772	382	44	426	1198
13	Wizara ya Biashara na Viwanda	132	70	202	32	19	51	253
14	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum	9196	4586	13782	1678	1209	2887	16669
15	Wizara ya Kilimo, Mali Asili na Uvuvi	1526	889	2415	509	168	677	3092
	JUMLA KUU	**19159**	**12700**	**31859**	**5461**	**3073**	**8534**	**40393**

Kiambatanisho nam 6b: Mashirika ya Umma

1	SHIRIKA LA BIASHARA	198
2	SHIRIKA LA UMEME	754
3	SHIRIKA LA NYUMBA	37
4	SHIRIKA LA BIMA	95
5	SHIRIKA LA UTANGAZAJI	343
6	SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA	44
7	SHIRIKA LA MAGAZETI	59
8	SHIRIKA LA BANDARI	420
9	PBZ	370
10	ZAWA	680
	JUMLA NDOGO	**3,000**

Kiambatanisho nam 6c: Shughuli za Tume ya Utumishi Serikalini kuanzia July, 2018 Hadi Kufikia Machi, 2019

WIZARA/TAASISI-	KUTHIBITISHWA KAZINI	NYONGEZA YA MUDA WA UTUMISHI	KUSTAAFU KWA MARADHI	KUSTAAFU KWA LAZIMA	KUSTAAFU KWA HIARI	LIKIZO BILA YA MALIPO	KUPANDISHWA DARAJA	KUBADILISHWA KADA	KUACHA KAZI	KUFUKUZWA KAZI
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	113	1	-	60	3	4	-	5	-	-
Wizara ya Fedha	17	2	-	1	-	1	20	8	-	1
Wizara ya Habari, na Mambo ya Kale	31	-	18	22	-	-	-	-	1	-
Wizara ya Vijana, Utamaduni utalii na michezo	2	-	-	6	-	1	-	1	-	-

Wizara ya Afya	1	-	14	207	4	1	-	13	2	12
Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, U/Umma na Utawala Bora	13	2	-	8	2	-	1	3	-	1
Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi	75	-	-	72	5	-	-	1	-	-
Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Mwenyekiti wa BLM	8	1	-	-	-	-	-	1	-	-
Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira	7	2	-	30	1	-	-	4	-	-
Wizara ya Biashara, Viwanda na masoko	4	3	-	-	-	-	-	-	-	-
Wizara ya Nchi ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	11	-	-	13	-	-	-	2	-	-

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	38	1	-	32	2	-	-	3	1	-
Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	6	1	-	10	1	-	-	1	1	-
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ	46	1	-	102	8	-	-	7	-	-
JUMLA KUU	**372**	**14**	**32**	**563**	**25**	**7**	**21**	**49**	**5**	**14**

Kiambatanisho nam 6d: Watumishi walioajiriwa Kuanzia Julai, 2018 Hadi Kufikia Machi, 2019

WIZARA / TAASISI		JUMLA
1	Wizara ya Afya	460
2	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	392
3	Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	10
4	Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa na Vikosi maalum vya SMZ	59
5	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto	69
6	Wizara ya nchi ofisi ya Rais, Katiba na Sheria	14
7	Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	59
8	Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira	53

9	Wizara ya nchi ofisi ya Makamo wa Pili wa rais	61
10	Wizara ya Vijana, Utamaduni, Utalii na Michezo	101
11	Wizara ya Fedha na Mipango	75
12	Mamlaka ya Kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi	52
13	Ofisi ya baraza la mapinduzi	5
14	Jeshi la kujenga uchumi Zanzibar	24
15	Tume ya Kurekebisha sheria	9
16	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	2
17	Tume ya Mipango	44
18	Ofisi ya Rais na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi	9

19	Wizara ya Kilimo, Maliasili mifugo na Uvuvi	72
20	Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki	23
21	Ofisiya Mufti Zanzibar	4
22	Idara ya Serikali mtandao	19
23	Kamisheni ya Utalii Zanzibar	13
24	Shirika la huduma za Maktaba	8
JUMLA		**1,637**

Kiambatanisho nam 6e: Malalamiko ya Watumishi kuanzia Julai–Machi 2018/19

Nam	WIZARA/TAASISI	IDADI YA WATUMISHI	AINA YA LALAMIKO LILILOWASILISHWA	UAMUZI ULIOFIKIWA NA TUME
1	Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili	1	Kuomba kurudishwa kazini	Madai yake yamekataliwa.
2	Wakala wa Uchapaji Serikalini	1	Kufutiwa kibali cha Uajiri	Dai limekataliwa.
3	Wizara ya Afya	1	Kuhamishwa wizara	Dai limekataliwa.
	JUMLA	**3**		